

Haki za Jamaa Zigeni za mupya Wakati wa Kushirikiana na Huduma za Ustawi wa Watoto

Haki za Wazazi na Walezi

Jamaa ziko na haki kama huduma za ustawi wa watoto zinahusika. Hizi haki zimewekwa kwa ajili ya kulinda jamaa yako na kuhakikisha kama unatendewa kwa haki. Uko na haki ya:

- **Kupata huduma za luga:** Uko na haki ya kupata mtafsiri na habari zenye zimetafsiriwa kama unazihitaji.
- **Kutendewa kwa heshima:** Utamaduni wako, imani zako, na mila za jamaa yako zinapashwa heshimiwa.
- **Kuelewa byenye biko na pitikana:** Unaweza kuuliza maswali na kuelezewa mambo mu luga yenye iko rahisi na ya kueleweka.
- **Kujua maswali yenye inahusika:** Uko na haki ya kujua ni juu ya nini huduma za ustawi wa watoto zinajihusisha na jamaa yako.
- **Kupima kuwaweka watoto wako kunyumba kama kuko salama:** Lengo la huduma za ustawi wa watoto ni kusaidia jamaa, hapana kuzitenganisha.
- **Kushiriki mu maamuzi:** Unaweza kusumulia juu ya hadisi yako na kuhusishwa kupanga mambo ya jamaa yako.
- **Kupata mwanasheria ao msaada wa kisheria mu kesi za ku mahakama:** Kama mahakama inahusika, uko na haki ya kupata uwakilishi wa kisheria.
- **Chunga habari zako kuwa siri:** Habari zako zinapashwa kubakia siri na zisishirikishwe na idara ya uhamiaji ao mashirika zingine bila ruhusa yako.



Haki za Watoto na Vijana

Watoto na vijana pia wako na haki wakati huduma za ustawi wa watoto zinahusika. Watoto na vijana wako na haki ya:

- Kukuwa **salama**
- Mahitaji yako, matakwa yako, na mapendeleo yako inapashwa sikilizwa na kuhesabiwa mu maamuzi.
- Kupata huduma mu jamii yako zenye zinalingana na mahitaji yako.
- Kupata **elimu na huduma za afya**.
- Kutendewa **kwa heshima**
- Kudumisha utamaduni **wao, luga yao, na mila zao**.
- **Kuendelea kuwasiliana** na wazazi, ndugu, na jamaa inapowezekana.
- Kupata **uwakilishi wa kisheria** na utetezi.
- Chunga habari **zako kuwa siri**

